



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA  
MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA  
NACHINGWEA**



Kumb. Na. LG.L.10/11/VOL.V/79

24 Mei, 2022

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Kwa kuzingatia kibali cha ajira Kumb.Na. FA.97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea anawatangazia Watanzania wenye sifa na uwezo kuomba ili kujaza nafasi 20 za kazi.

**1. MTENDAJI WA KIJIKI III NAFASI KUMI NA SITA (16)  
SIFA ZA MWOMBAJI**

- Muombaji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyefuzu mafunzo ya Astashahada/Cheti, "NTA level 5" katika fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii, kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI**

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao
- Kuwa Mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- Kuratibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake.
- Kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wataalam katika Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za vijiji.

**MSHAHARA**

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kina mshahara wa TGS B

## 2. DEREVA DARAJA LA II-NAFASI NNE (04)

### KAZI NA MAJUKUMU YA DEREVA II

- Kukagua gari kabla na baada ya Safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kufanya na kusambaza nyaraka mbalimbali pale inapohitajika
- Kujaza na kutunza taarifa ya za safari zote katika daftari la safari
- Kufanya usafi wa gari na
- Kazi nyingine atazopangiwa na mwajiri

### SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe amehitimu kidato cha IV/VI
- Awe na Leseni daraja "E au C1" na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali .
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- Muombaji mwenye cheti cha majaribio ya Ufundi daraja la II atafikiriwa kwanza

### MSHAHARA

Cheo cha Dereva Daraja la II kina mshahara wa TGS B

### MASHARTI YA JUMLA

- i. Muombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutumwa kupitia anuani iliyotajwa hapo chini.
- iii. Muombaji ambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iv. Muombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma na ana sifa za kuingilia katika kada tofauti na aliyonayo apitishie barua yake ya maombi kwa mwajiri wake kuthibitisha kuridhia.
- v. Muombaji aambatishe maelezo binafsi yaliyojitokeza (a detailed C.V) yenye anuani, namba za simu, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- vi. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali:-
  - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV au VI.
  - Cheti cha mafunzo (professional).
  - Cheti cha kuzaliwa.
  - Picha moja (1) "passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vii. "Testimonials", "Provisional results", Statement of results", hati matokeo za kidato cha IV na VI (form IV nad form VI result slips) **HAVITAKUBALIWA.**

- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahusika kushughulikiwa kisheria.
- ix. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 06/06/2022 saa 9.30 alasiri.
- x. Watakaoitwa kwenye usaili majina yao yatawekwa kwenye tovuti ya Halmashauri ([www.nachingweadc.go.tz](http://www.nachingweadc.go.tz))
- xi. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza na yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA  
S.L.P 291,  
NACHINGWEA.

Limetolewa na:-



Eng. Chionda A. Kawawa  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
NACHINGWEA



MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
NACHINGWEA

*Jiandae kuhesabiwa siku ya jumanne tarehe 23 Agosti, 2022*

- NAKALA:- - Mbao za matangazo
- Tovuti: [www.nachingweadc.go.tz](http://www.nachingweadc.go.tz)